

Kwa ajili ya usalama wa wanafunzi, familia na wafanyakazi, wazazi watakuwa na nafasi ya kuchagua jinsi wangependa mtoto wao asome kwa kuchagua mtindo mmoja kati ya mitatu katika mwaka wa masomo wa 2020-21.

Mtindo #1: Mtindo wa Kusomea Shuleni – 100% Uso-kwa-Uso

Kurudi kwa wanafunzi na wafanyakazi wote kwa majengo ya shule “kama kawaida” kutafanya shughuli za kuosha na usafi ziongezeke kama itakavyoelezewa baadaye katika mwongozo huu. Tafadhali tambua- chaguo hili **HALIPO** kwa sasa kwa kuwa haliwezi kuhakikisha umbali kati ya mtu mmoja na mwingine pamoja na hatari iliyopo ya maambukizi ya virusi katika jamii kwa wakati huu.

Mtindo#2: Mtindo Mseto wa Masomo – Uso-kwa-Uso 50% ya muda wa masomo, mtandaoni 50% ya muda wa masomo

Ili kupunguza idadi ya wanafunzi darasani wakati wa masomo ya uso kwa uso, wanafunzi watafuata mpangilio mmoja kati ya miwili iliyoonyeshwa hapa chini. Itahakikishwa kwamba kuna ongezeko la shughuli za kusafisha na usafi kama itakavyoelezewa baadaye katika nakala hii. *Tambua: huu ndio mtindo wa kimsingi ambao utatumika mwanzoni mwa mwaka wa shule wa 2020/2021 kulingana na jina la mwisho la familia inayohusiana na mwanafunzi. Kundi la A litajumuisha majina ya mwisho ya familia yanayoanzia na herufi A-K. Kundi la B litajumuisha majina ya mwisho yanayoanzia na L-Z.

		Wiki 1					Wiki 2				
		J	J	J	A	I	J	J	J	A	I
Kundi A		Shuleni	Shuleni	Shuleni	Nyumbani mtandaoni	Nyumbani mtandaoni	Shuleni	Shuleni	Nyumbani mtandaoni	Nyumbani mtandaoni	Nyumbani mtandaoni
Kundi B		Nyumbani mtandaoni	Nyumbani mtandaoni	Nyumbani mtandaoni	Shuleni	Shuleni	Nyumbani mtandaoni	Nyumbani mtandaoni	Shuleni	Shuleni	Shuleni

*Wakati wa mtindo mseto, K-12 watakuwa na masaa 6 na dakika 25 za kusoma na hawatakuwa wakitoka shuleni mapema Jumatano kila wiki. Shule ya Elementary itaanzia 8:00-2:25, Junior High School itaanzia 9:10 - 3:35 na High School itaanzia 8:35 - 3:00.

Mtindo#3: Mtindo wa Kusomea Mtandaoni-Pekee (Haya SI masomo ya nyumbani.)

Wanafunzi katika mtindo huu watapokea 100% ya masomo yao kupitia njia ya mtandao. Mahudhurio na kukamilisha mazoezi ni lazima. Wanafunzi wataendelea kusajiliwa kutoka majengo yao ya nyumbani na wataendelea kuwasiliana na walimu wa DCSD na wafanyakazi ili kuelekeza masomo yao.

*Muhimu: punde tu utakapochagua Mtindo wa Masomo ya Mtandaoni Pekee, mtoto wako atalazimika kusomea mtandaoni muhula mzima. Kwa gredi K-8, muhula wa kwanza utakamilika Januari 29. Kwa gredi 9-12, muhula wa kwanza utakamilika Februari 17. Mtakuwa na fursa ya kuchagua mtindo mseto wa masomo ya shuleni na mtandaoni mwanzoni mwa muhula wa pili na mnaweza kuchagua kuhamisha wanafunzi wenu kwa Chaguo#3 wakati wowote.